

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAMISEMI



NAMBA ZA SIMU:

MKUU WA SHULE: +255755925011/0782534488

MAKAMU MKUU WA SHULE: +255762842080

PATRON: +255757675345.

Email.runzewesec@g.mail.com

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....

S.L.P.....

Shule Ya Sekondari Runzewe

S.L.P 55,

BUKOMBE

TAREHE 01/06/2018

YAH : MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE - HALMASHAURI YA BUKOMBE MKOA WA GEITA MWAKA 2018.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya_____. Shule ya Sekondari Runzewe ipo umbali wa kilimita 55 Magharibi ya mji wa Ushirombo. Usafiri wa basi kutoka mjini Ushirombo unapatikana katika kituo cha mabasi Ushirombo. Pia unaweza kufika katika mji wa Runzewe moja kwa moja kutoka sehemu yoyote ya Tanzania.

Muhula wa masomo unanza tarehe 02/07/2018, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shulen tarehe 02/07/2018, mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/07/2018.

2. Mambo muhimu ya Kuzingatia:

2.1 Sare ya Shule.

- a) Sare ya Shule hii ni suruali mbili (2) za rangi nyeusi isiyo na michilizi yoyote na yenye mifuko miwili (2) pembeni na nyuma mmoja (1) isiwe "Modal style" Mashati mawili (2) meupe tetroni Yenye mikono mirefu.
- b) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
- c) Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi.
- d) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
- e) Sare ya michezo ni raba, bukta, tsheti au jezi. (Rangi ya bluu)
- f) Nguo za kushindia (Shamba dress) ni mashati mawili (2) ya rangi ya damu ya mzee, mashati hayo yawe ya mikono mifupi na yasiwe na urembo/mapambo au kudariziwa na Suruali nyeusi iliyoelezwa kwenye kipengele (a).
- g) Tracksuit moja (1) ya rangi ya bluu.
- h) Sweta moja (1) la rangi ya kijani jeshi lenye mstari mweupe kifuani.
- i) Tai ndefu ya rangi ya damu ya mzee.
- j) Tsheti moja (1) ya rangi ya bluu yenye kora nyeupe.

ANGALIZO:

Nguo tofauti na hizo zilizotajwa hapo juu hazitakiwi kabisa shuleni. Sare zilizopo katika kipengele (h) - (j) zinapatikana shuleni kwa gharama zifuatazo:

- i. Sweta Tshs. 15,000/=
- ii. Tsheti Tshs. 10,000/=
- iii. Tai Tshs. 2,000/=

Michango hii ilipwe shuleni sio bank

2.2 Ada na Michango ya Shule.

- a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs 70,000/=, unaweza kulipa kiasi cha Tshs. 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti Na. **3251200066** jina la akaunti Runzewe Secondary School Current Account Benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).
- b) Michango ya shule
- i. Ukarabati wa Samani Tsh. 15,000/=
 - ii. Kitambulisho Tshs. 6,000/=
 - iii. Taaluma Tshs. 20,000/=
 - iv. ulinzi Tshs. 30,000/=
 - v. Nembo ya shule Tshs. 2,000/=
 - vi. Matibabu Tshs. 10,000/=
 - vii. Mpishi Tshs. 20,000/=
 - viii. Maji Tshs. 20,000/=
 - ix. Tahadhali Tshs. 5,000/=
 - x. Mock. 15,000/=
- JUMLA TSHS 143,000/=.**

Fedha hii ya michango ilipwe kwenye akaunti Na. **3256600010** jina la akaunti Runzewe Secondary School Revenue Collection Benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

c) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni:**

- i. Faili moja (folder file)
- ii. Jembe lenye mpini, kwanja, ndoo ya lita 10, hardbloom na softbloom.
- iii. Ream ya karatasi A4 (kwa mwaka).
- iv. Godoro futi $2\frac{1}{2}$ x 6 na chandarua.
- v. Mashuka pair 2 ya rangi ya pink na blanketi la rangi yoyote.
- vi. Sanduku imara la chuma lenye kufuli.
- vii. Scientific calculator kwa wanafunzi wa mchepuo wa PCB.
- viii. Sahani, bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula.
- ix. Ndoo moja (ya lita 20) kwa ajili kutunzia maji na usafi binafsi.
- x. Beseni au dishi kwa ajili ya kuogea na usafi.
- xi. Vifaa vingine vya kutosha vinavyokubalika shuleni kwa matumizi binafsi kwa muhula mzima. Mfano: sabuni, madaftari, vitabu vya masomo husika n.k
- xii. Picha. (passport size) 4, 2 za wazazi/walezi na 2 na ndugu wa karibu na mwanafunzi watakaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

ANGALIZO.


Fomu zifuatazo zinatakiwa kurudishwa shuleni zikiwa zimejazwa, vizuri,

- i. Fomu maalumu kwa wanafunzi.
- ii. Fomu ya kiapo cha kutomiliki simu shuleni.
- iii. Fomu ya vipimo vya mwanafunzi (vipimo vithibitishwe na Daktari wa Hospitali ya serikali).

3. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

- i. Wizi
- ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
- iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
- iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
- v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
- vii. Kufuga ndevu.
- viii. Ulevi na unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevywa.
- ix. Uvutaji wa sigara.
- x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoja au kuolewa.
- xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
- xii. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
- xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- xv. Kumiliki, kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- xvi. Kudharau bendera ya taifa
- xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
- xviii. Uharibufu wa mali za Umma kwa makusudi.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



R.B. HALILI

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI RUNZEVE
S.L.P. 55
BUKOMBE - GEITA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE.

SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE

.S.L.P 55 – BUKOMBE-GEITA.

MEDICAL EXAMINATION FORM

PART A: TO THE MEDICAL OFFICER.

Name of student.....

Kindly, examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for being registered into full time ordinary secondary studies.

S/N	EXAMINATION CONDITIONS	STATUS/ REMARKS
1	Physical abnormality	
2	Hearing ability	
3	Urine	
4	Stool	
5	Tuberculosis	
6	Psychosis	
7	Epilepsy	
8	Sight	
9	Blood pressure	
10	Speech	
11	Pregnance	

Any other health problem _____

PART B: (To be completed by the Government medical officer)

I have examined the condition of the student and consider that he/she is **FIT/ UNFIT** to pursue this level of studies.

DATE..... SIGNATURE.....

STATION.....DESIGNATION.....

4. KUHUSU MWANAFUNZI KUMILIKI SIMU SHULENI.

Kikao cha bodi ya shule cha tarehe 17.08.2017 kilikubaliana na adhabu zifuatazo kwa mwanafunzi atakae kamatwa na simu shuleni:-

1. Kuchapwa viboko vinne 4 mbele ya wanafunzi wate mstarini.
2. Kusimamishwa masomo siku 21
3. Siku ya kurudi shuleni mwanafunzi atatakiwa kuja na mzazi /mlezi wake na faini ya shilingi laki mbili(TSH. 200000).
4. Simu na kadi ya simu vitavunjwa mbele ya wanafunzi na mzazi/mlezi.

N.B Endapo mzazi/mlezi atashindwa kutekeleza vipengele tajwa (i-iv) mwanafunzi atafukuzwa shule.

JINA LA MWANAFUNZI _____ SAHIHI _____

TAREHE _____

H'ALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

SHULE YA SEKONDARI RUNZEWE

S.L.P 55 BUKOMBE – GEITA

FOMU MAALUMU KWA MWANAFUNZI

1. MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI:

- (i) Jina la Mwanafunzi _____ Jinsia _____ Tarehe ya kuzaliwa _____
- (ii) Shule ya Msingi/Sekondari aliyotoka _____
- (iii) Jina la Baba _____ Kazi yake _____ Na. ya simu _____
- (iv) Jina la Mama _____ Kazi yake _____ Na. ya simu _____
- (v) Kijiji/Mtaa wanapoishi _____ Wilaya _____ Mkoa _____
- (vi) Dini _____
- (vii) Majina ya ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutoa msaada pindi wanapohitajika:
- a) _____ anakoishi _____ Na. ya simu _____
- b) _____ anakoishi _____ Na. ya simu _____
- c) _____ anakoishi _____ Na. ya simu _____
- d) _____ anakoishi _____ Na. ya simu _____
- (viii) Michezo anayoweza kushiriki mwanafunzi shuleni: _____

NB: Je wazazi wote wako hai? *Ndiyo/Hapana (*Kata isiyositahili)
Kama amefariki/wamefariki, aliyefariki ni _____

2. KUKUBALI NA KUTII SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE:

Mimi (Jina la Mwanafunzi) _____ naahidi sitashiriki kabisa katika fujo/migomo na kutenda makosa ya jinai shuleni na maeneo mengine. Pia, naahidi kuzifuata taratibu na sheria zote za shule kwa faida yangu binafsi, shule na Taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na taratibu na kanuni za shule nakubali kufukuzwa shule, kusimamishwa masomo na kufikishwa mahakamani au kupewa adhabu nyingine kulingana na sheria.

JINA LA MWANAFUNZI _____ SAHIHI _____ TAREHE _____
JINA LA MZAZI/MLEZI _____ SAHIHI _____ TAREHE _____

3. MZAZI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA KUTEKELEZA MAELEKEZO YA SHULE:

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi) _____ nakubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada na michango yote kwa wakati mwafaka na kutekeleza maelekezo yatolewayo na shule.

Vilevile, naahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa uongozi wa shule pindi nikihitajika kuhusu tabia, mwenendo au suala jingine lolote linalomhusu mtoto wangu.

JINA LA MZAZI/MLEZI _____ SAHIHI _____ TAREHE _____


MKUU WA SHULE

FOR HEADMASTER
RUNZEWE SEC. SCHOOL
P.O. BOX 55
BUKOMBE - GEITA